

Mitandao ya Kijamii na Kushiriki

Washiriki wataangazia faragha kulingana na jinsi wanavyoshiriki maelezo na kuwasiliana na watu wengine mtandaoni, hususan kuhusiana na matumizi ya mitandao ya kijamii. Wataweza kueleza mifaka ya kibiashara faraghani katika muktadha wa mitandao ya kijamii na kujifunza jinsi ya kutumia ipasavyo mipangilio ya faragha mtandaoni.

Matumizi ya Mitandao ya Kijamii

Sehemu ya Kwanza

Mwingiliano wa Darasa

Kabla ya shughuli inayofuata, weka ishara ya “KUBALI” na “KATAA” kwenye sehemu mikabala ya chumba. Wajulishe washiriki kwamba mara tu ukishasoma kila kauli, wanafaa kusimama sehemu moja au nyingine kwa kutegemea jinsi wanavyohisi; washiriki pia wanaweza kusimama katikati ya ishara zile mbili ikiwa hawana uhakika / wameshindwa kuamua.

Unaposoma kauli zile, waulize wahusika waeleze misimamo yao na uwahusishe katika mijadala mifupi kwenye kikundi kuhusu kila mada.

Ambia Wanafunzi Wako

Nitasoma taarifa. Ikiwa unakubaliana nayo asilimia mia moja, nenda usimame kwenye ishara ya “KUBALI”. Ikiwa unakataa kabisa, nenda usimame kwenye “ISHARA” ya “KATAA”. Ikiwa huna uhakika au hukubaliani / unakataa kabisa, nenda usimame kwenye sehemu ya katikati katika nafasi inayowakilisha maoni yako ifaavyo.

Nina akaunti kwenye mitandao ya kijamii kama vile Facebook, Twitter, Snapchat au Instagram.

Ninatumia mitandao ya kijamii kila siku.

Wasifu wangu kwenye mitandao ya kijamii – kwenye jukwaa la mtandao wa kijamii ninaotumia zaidi – huonekana kwa umma.

Nina marafiki tofauti / wafuasi / watu ninaounganishwa nao (yaani, hadhira tofauti) kwenye majukwaa mbalimbali ya mitandao ya kijamii ninayotumia.

Kizazi changu wana njia tofauti ya kufikiria kuhusu maelezo yanayoshirikiwa kwenye majukwaa ya mitandao ya kijamii wakilinganishwa na watu wazima.

Ninatumia majukwaa tofauti ya mitandao ya kijamii kuchapisha aina mahususi ya maudhui.

Upeo wa Maombi ya Urafiki

Sehemu ya Kwanza

Ambia Wanafunzi Wako

Jukwaa la mtandao wa kijamii ni jukwaa la mtandaoni unaloweza kutumia kuwasiliana na watu na kutagusana nao.

Uliza Wanafunzi Wako

Je, ni majukwaa yapi ya mtandao wa kijamii ambayo umesikia kuyahusu?

Sehemu ya Pili

Mwingiliano wa Darasa

Kabla ya shughuli ifuatayo, weka ishara ya “KUBALI” na “KATAA” kwenye sehemu mikabala ya chumba. Wajulishe washiriki kwamba mara tu ukishasoma kila kauli, wanafaa kusimama sehemu moja au nyingine kwa kutegemea jinsi wanavyohisi; washiriki pia wanaweza kusimama katikati ya ishara mbili ikiwa hawana uhakika / wameshindwa kuamua.

Katikati ya taarifa, washirikishe wanakikundi kwenye mijadala mifupi ukitumia maswali yaliyo chini ya kila kauli.

Ambia Wanafunzi Wako

Nitasoma taarifa. Ikiwa unakubaliana nayo asilimia mia moja, nenda usimame kwenye ishara ya “KUBALI”. Ikiwa unakataa kabisa, nenda usimame kwenye “ISHARA” ya “KATAA”. Ikiwa huna uhakika au hukubaliani / kukataa kabisa, nenda usimame kwenye sehemu ya katikati katika nafasi inayowakilisha maoni yako ifaavyo.

Kwa ajili ya shughuli hii, fikiria kuhusu akaunti ya mtandao wa kijamii unayotumia zaidi.

Uliza Wanafunzi Wako

Wasifu wangu kwenye mitandao ya kijamii unaonekana kwa umma.

1. Je, hali hii hubadilisha jinsi unavyochapisha mambo mtandaoni? Kivipi? Au ikiwa sivyo, kwa nini?

Wasifu wangu kwenye mitandao ya kijamii unaonekana kwa marafiki / watu

ninaowafahamu vyema pekee.

1. Kwa nini ulifanya uamuzi huu?
2. Ikiwa watu wote wangeweza kuona wasifu wako, je ungechapisha mambo tofauti? Mambo aina gani?

Nina rafiki / mfuasi / mtu niliyeunganishwa naye kwenye mitandao ya kijamii ambaye sijawahi kutana naye maishani.

1. Kwa nini uliamua kuwa rafiki / kumfuata / kuunganishwa na mtu huyu? Je, ni mtu ambaye ulikutana naye mtandaoni au hamjawahi kutana hapo awali?
2. Je, unaweza kueleza vipi uhusiano wenu?
3. Kwa sababu mnawasiliana tu mtandaoni, je, hiyo hushawishi namna mnavyotagusana? Je, baadhi ya manufaa ya aina hii ya mtagusano ni yepi? Je, changamoto zipi zinaweza kuwepo?

Uliza Wanafunzi Wako

Mimi hukubali kila ombi la urafiki / mfuasi / mtu wa kuunganishwa naye ninalopata.

1. Je, manufaa ya mwelekeo huu ni yepi? Je, changamoto zipi zinaweza kuwepo?
2. Je, wewe hutilia maanani faragha unapopokea maombi ya urafiki / mfuasi / mtu uliyeunganishwa naye? Ikiwa ndiyo, vipi? Ikiwa sivyo, kwa nini?

Kila nikikutana na watu wapya, huwa ninawatumia ombi la urafiki / kuwafuata / kuunganishwa nao.

1. Kwa nini wazo hili ni njema / si njema?

Nimefuta marafiki / wafuasi / watu niliunganishwa nao.

1. Kwa nini ulifanya uamuzi huu?

Uliza Wanafunzi Wako

Mtandaoni, mimi ni rafiki na / ni mfuasi wa / nimeunganishwa na wazazi wangu / walezi au walimu.

1. Je, hali hii hubadilisha jinsi unavyochapisha?
2. Je, watu wazima walio maishani mwako hutoa maoni kuhusu mambo unavyochapisha mtandaoni?
3. Je, manufaa ya na / au changamoto za kuwa rafiki / kuwafuata / kuwasiliana na wazazi wako / walezi au walimu wako ni yapi?

Baadhi ya mambo kwenye wasifu wangu yanaweza kuonekana na marafiki wa marafiki / watu ambao sijaunganishwa nao moja kwa moja kwenye mtandao wa kijamii.

1. Mambo yepi?

Nimeangalia na / au nimebadilisha mipangilio yangu ya faragha.

1. Kwa nini au kwa nini hukufanya hivyo?
2. Je, mipangilio hii ya faragha ni rahisi au inakanganya? Je, nini ingefanya mipangilio hii kuwa rahisi zaidi kuona / kubadilisha?

Je, Mtandao wako ni Mkubwa Kiasi Gani?

Sehemu ya Kwanza

Ambia Wanafunzi Wako

Sasa tuzungumze jinsi ambavyo unaweza kuchagua nini uwashirikishe wenzako wakati unatumia mitandao ya kijamii.

Kuna njia mbili kuu katika hali ya maudhui yapi (k.m., picha, video, chapisho linalozingatia matini) yanashirikiwa na hadhira. Kwanza, maudhui yanaweza kushirikiwa na hadhira chaguo-msingi, ambayo inaweza kuwa marafiki zako / wafuasi / wale uliunganishwa nao tu, au inaweza kujumuisha marafiki za marafiki vilevile. Pili, hadhira yako ya kwanza inaweza kushiriki maudhui na marafiki zao / wafuasi / wale waliunganishwa nao.

Unaweza kuchagua hadhira yako ya karibu lakini ni vigumu zaidi kudhibiti ni nani hadhira yako inashiriki upya / kuchapisha upya / au kutuma tweet maudhui upya.

Uliza Wanafunzi Wako

Chukulia kuwa umeshiriki maudhui sio na marafiki / wafuasi / wale ambao umeunganishwa nao tu, lakini maudhui hayo pia yanashirikiwa na marafiki zao / wafuasi / wale waliunganishwa nao, unafikiria ni watu wangapi unashiriki nao?

Sehemu ya Pili

Mwingiliano wa Darasa

Andika hesabu/matokeo yafuatayo ubaoni.

Ambia Wanafunzi Wako

Hebu tufanye hesabu kidogo. Iwapo, kwa mfano, una marafiki / wafuasi / miunganisho miwili kwenye jukwaa la mtandao wa kijamii, na kila moja ina marafiki / wafuasi / miunganisho mitatu, hivyo ni watu wangapi, kwa idadi ya juu zaidi (baadhi yao marafiki wanaweza kupitana) wanaweza kuona maudhui unayoshiriki kwenye jukwaa?

1. Jibu: $2 + 2 \times 3 = 8$

Iwapo, kwa mfano, una marafiki / wafuasi / miunganisho kumi kwenye jukwaa la mtandao wa kijamii, na kila moja ina marafiki / wafuasi / miunganisho kumi, hivyo ni watu wangapi, kwa idadi ya juu zaidi wanaweza kuona maudhui unayoshiriki kwenye jukwaa?

1. Jibu: $10 + 10 \times 10 = 110$

Iwapo, kwa mfano, una marafiki / wafuasi / miunganisho mia tatu kwenye jukwaa la mtandao wa kijamii, na kila moja ina marafiki / wafuasi / miunganisho mia tatu, hivyo ni watu wangapi, kwa idadi ya juu zaidi wanaweza kuona maudhui unayoshiriki kwenye jukwaa?

1. Jibu: $300 + 300 \times 300 = 90,300$

Ambia Wanafunzi Wako

Ukokotoaji huu ulizingatia dhana kuwa hadhira yako ya karibu zaidi inashiriki maudhui na hadhira yao ya karibu, lakini hakuna kushiriki kwa ziada kunakofanyika baada ya hapo. Hata hivyo, katika hali nyingi, maudhui yanaweza kushirikiwa vizuri mbali na hadhira hizo mbili za karibu zaidi.

Sehemu ya 3

Uliza Wanafunzi Wako

Je, unahisi vipi kuhusu uwezekano kwamba watu ambao pengine huwafahamu (huenda unawafahamu baadhi ya marafiki wa marafiki zako) wanaweza kufahamu kwa urahisi shughuli zako mtandaoni? Je, ni mambo yepi yanaweza kuwa ni nguzo bora / zisizo bora kuhusu suala hili?

Je, kwa nini jambo hili ni muhimu?

Je, jambo hili linabadilisha jinsi unavyofikiria kuhusu kushiriki mambo mtandaoni? Kwa nini ufanye au usifanye hivyo?

Kushiriki Mtandaoni

Mjadala wa Kwanza

Ambia Wanafunzi Wako

Unaweza kuweka habari zako katika mitandao ya kijamii kwa ajili ya hadhira lengwa lakini unapoweka katika umma, yale utakayowashirikisha wenzako yanaweza kupata kutizamwa na wale usiowatarajia.

Maudhui yanayoshirikiwa yanaweza “kusambaa,” mtandaoni kwa kasi kwenye mitandao ya kijamii, kuigwa au ikiwezekana kuandaliwa upya.

Uliza Wanafunzi Wako

Je, kuna yeyote anayeweza kufikiria kuhusu mfano wa maudhui yaliyosambaa mtandaoni?

1. Ikiwa sivyo, waulize wafikirie kuhusu picha za kuchekesha, maandalizi mapya au video maarufu ambazo wameona na / wameshiriki na marafiki zao.

Muingiliano

Mwingiliano wa Darasa

Onyesha mfano wa sasa uliolinganishwa na muktadha wa ndani / kieneo ambao ni wako / wa mshirika ili kuimarisha zaidi dhana hiyo.

Mjadala wa Pili

Ambia Wanafunzi Wako

Maudhui yaliyosambaa yanaweza kuwa mazuri ikiwa unataka kazi yako iangaziwe zaidi. Hata hivyo, maangazio yanaweza kuwa unyanyasaji na dhuluma mtandaoni. Video ya kisiri ambayo inasambazwa au kushirikiwa bila idhini yako inaweza kuvuruga sifa yako.

Uliza Wanafunzi Wako

Je, maudhui kuu kuhusu mtandaoni yanaweza kushirikiwa vipi kupita hadhira yako lengwa na hali hii inawezaje kukuathiri na / au sifa yako?

Namna ya kujisitiri wakati ukitumia mitandao ya kijamii/Jinsi ya kuficha baadhi ya taarifa zako wakati ukitumia mitandao ya kijamii

Sehemu ya Kwanza

Ambia Wanafunzi Wako

Kwa vile sasa tumezungumza kuhusu baadhi ya sababu zinazokupelekea usitake kila kitu unachofanya mtandaoni kuwa kwenye umma, hebu tuzungumze kuhusu jinsi ya kudhibiti faragha yetu mtandaoni.

Sehemu ya Pili

Mwingiliano wa Darasa

Unapouliza maswali, fafania zaidi mjadala kwa kutumia kauli zilizo chini ya kila swali.

Ambia Wanafunzi Wako

Je, kuna maana ya kuwepo kwa mipangilio tofauti ya faragha kwa aina tofauti za maelezo?

1. Unaweza kuzingatia maelezo tofauti kuwa yana viwango tofauti vya faragha. Unaweza kupenda kushiriki na hadhira tofauti picha ya uso wako, tweet kuhusu imani yako ya kisiasa au kidini au habari kuhusu video ya kuchekesha.

Je, vipi kuhusu mipangilio tofauti ya faragha kwa ajili ya watu tofauti? Kwa mfano, wazazi wako / walezi na marafiki huweza kuona mambo sawa kwenye akaunti zako za mitandao ya kijamii?

1. Huenda washiriki hawataki wanafamilia zao kuweza kutoa maoni kwenye machapisho yao japo wangependa marafiki zao kutoa hisia zao.

Je, ungependa kurudi na kuangazia upya kila kitu ambacho umehusishwa nacho? Kwa nini au kwa nini hukufanya hivyo?

1. Unaweza kutaka kuondoa maudhui yoyote ya kuaibisha (m.f., picha ya siku ya nywele mbovu, chapisho kukuhusu ambalo hutaki lishirikiwe).

Kwenye majukwaa mengine ya mitandao ya kijamii kama vile Facebook, unaweza

kubadilisha mipangilio yako hivi kwamba utaweza kuhalalisha jambo kabla halijaonekana kwenye wasifu wako. Je, unafikiri hilo ni wazo nzuri? Kwa nini, kwa nini sio?

1. Inakusaidia kuzuia maudhui ya kuaibisha kuambatishwa kwenye akaunti yako ya mtandao ya kijamii. Hata hivyo, haimzuii mtu anayechapisha maudhui kuyashiriki kwenye akaunti zake na marafiki / wafuasi / watu waliunganishwa nao.

Kwa nini mtu anaweza kubana watu wanaoweza kumwangalia? Je, unaweza kutoa mfano?

1. Huenda hutaki wageni / watu usiowafahamu vyema kuwa rafiki / kukufuata / kuungana nawe kwenye mitandao ya kijamii au kukutumia ujumbe ambao hujaulizia.

Je, wewe ni rafiki na / mfuasi wa / umeunganishwa na wazazi / walezi wako mtandaoni? Je, walimu? Watu wengine wazima?

1. Je, hali hii hubadilisha aina ya maudhui unayoshiriki na watu unaoshiriki nao?

Je, wazazi / watunzaji au walimu wanahitaji kuwa rafiki nawe/ kuwa wafuasi wako / kuunganishwa nawe ili waweze kuona wasifu wako?

1. Washiriki wanapaswa kuzingatia ikiwa mipangilio yao ya kibinafsi ya faragha huruhusu umma kwa jumla kuona wasifu wao wa mitandao ya kijamii. Wasaidie kutafakari kuhusu njia mbadala ambazo wazazi / walezi au walimu wanaweza kutumia kuona wasifu wao.

Na je, mipangilio tofauti ya faragha kwenye majukwaa tofauti ya mitandao ya kijamii? Je, kwenye mtandao wa Twitter, tweet zako huonekana kwa umma au huwa ni za faragha? Je, watu wangapi wanaweza kuona hadithi zako kwenye Snap? Watu wangapi wanaweza kufikia habari kwenye mtandao wako wa Instagram? Je, watu wengine wanaweza kuona video zako kwenye YouTube? Je, watu wanaweza kuona picha zako kwenye Facebook, kando na picha yako kwenye wasifu?

1. Ikiwa washiriki hawafahamu, waambie kwamba kuna mipangilio ya faragha ya masuala haya.

Je, wewe hutuma tweet kwa kutumia jina lako halisi au jina bandia? Kwa nini?

1. Huenda washiriki hawataki umma kwa jumla ifahamu majina yao halisi. Katika

hali hii, huenda wangependa kutumia jina bandia.

Sehemu ya Tatu

Mwingiliano wa Darasa

Waandae washiriki katika jozi.

Ambia Wanafunzi Wako

Tunafahamu kwamba mipangilio ya faragha inaweza kukanganya.

Kwenye vikundi vyenu, chukua dakika chache ili kuandaa swali au maoni kuhusu mipangilio ya faragha.

Mwingiliano wa Darasa

Wape washiriki dakika 5 ili waweze kuandaa swali au maoni kuhusu mipangilio ya faragha. Waulize washiriki pamoja na kikundi kizima na wajibu kila swali lililoulizwa. Waulize washiriki majibu yao kabla hujatoa jibu lako.

Ikiwa kuna kompyuta au vifaa vya mkononi vinavyoweza kufikia mtandao, onyesha jinsi ya kudhibiti mipangilio ya faragha mtandaoni.

Kazi

Mwongozo

Ambia Wanafunzi Wako

Kwa vile sasa tumezungumza kuhusu faragha kwenye mitandao ya kijamii, hebu tuendeleze hayo kwa kuunda mwongozo unaoweza kutumika kuwasaidia watu wengine kujifunza yale ambayo umejifunza.

Kwa muda wa dakika 30 zijazo, andaa mwongozo mfupi wewe binafsi ili kuwasaidia watu wengine:

1. Waza kuhusu hadhira wanaolenga wanapochapisha kwenye mitandao yao ya kijamii.
2. Tafakari kuhusu mambo yale wangependa kushiriki kwenye umma na yale ambayo wangependa kuweka faraghani na kwa nini?
3. Zingatia ni kwa nini huenda wangependa kuangazia upya na / au kubadilisha mipangilio yako ya faragha kwenye mitandao ya kijamii.
4. Waza jinsi wanavyoweza kuweka mipangilio tofauti ya faragha kwa maudhui tofauti na kwa nini wangependa kufanya hivyo.

Mwongozo huu unaweza kuandaliwa katika muundo unaopenda. Unaweza kuandika mwongozo unaofuata hatua baada ya nyingine, isanifu kama “mwongozo wa mtumiaji,” jumuisha picha pamoja na chati mtiririko au mbinu nyingine ambazo unafikiria zinaweza kuwasaidia watu wengine kujifunza mambo haya; kuwa huru kuwa mbunifu! Kwenye mwongozo huu, hakikisha pia kwamba:

1. Umewaonyesha wasomaji jinsi ya kuangazia upya na kubadilisha mipangilio ya faragha kwenye jukwaa la mtandao wa kijamii.
2. Toa jibu kwa swali kuhusu mipangilio ya faragha unaloamini kuwa ni muhimu kulingana na mijadala iliyopita ya kikundi.

Utoaji

Wahimize washiriki ili wachague majukwaa tofauti ili kwa pamoja majukwaa mengi yaangaziwe. Wape washiriki dakika 30 ili wakamilishe kazi.